# Wafugaji Rombo wapata neema ya soko la maziwa

**Janeth Joseph**, Mwananchi
jjoseph@Mwananchi.co.tz

**Rombo.** Wafugaji wa vijiji vya Shimbi na Keni wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro waliokuwa wakitembea zaidi ya kilomita 20 kutafuta soko la maziwa, sasa wameondokana na adha hiyo baada ya kufunguliwa kituo cha kuuzia bidhaa hiyo.

Awali, wafugaji hao walikuwa wakitembea umbali mrefu kwenda kutafuta soko la maziwa katika nchi jirani ya Kenya kutokana na kukosekana kwa mnunuzi wa maziwa hayo.

Kituo hicho cha maziwa kilichofunguliwa na Kiwanda cha Kondiki kilichopo eneo la Shimbi, kina uwezo wa kukusanya lita 500 za maziwa kwa siku.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wafugaji hao walisema kwa miaka mingi wamekuwa wakifuga bila tija, licha ya kutumia gharama kubwa kutokana na kukosekana kwa soko la uhakika la maziwa.

Walisema walikuwa wakiuza maziwa kwa hasara na wakati mwingine walikwenda kuuzia nchi jirani ya Kenya kwa Sh800 kwa lita.

Edward Massawe, ambaye ni mfugaji wa ng'ombe wa maziwa wilayani humo, alisema kutokuwa na vikundi vya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa wilayani humo imekuwa ni changamoto kubwa na kwamba ndiyo sababu ya wao kutozalisha kwa tija.

"Changamoto tuliyonayo ni kutokuwa na vikundi vya wafugaji, hasa wa ng'ombe wa maziwa, kutokana na hali hii ilitulazimu kuchukua maziwa hapa na kwenda kuyauza Kenya kwa sababu hakuna soko la uhakika na tulikuwa hatuna pakuuzia maziwa tunayozalisha hapa kwetu," alisema Massawe.

"Ukiangalia gharama ya maziwa iko chini sana, unakuta tunauza maziwa Sh800 kwa lita moja, kwa bei hiyo inamtia hasara mfugaji, maana zile gharama unazozitumia katika uzalishaji hazirudi, hivyo wakati mwingine mkulima analazimika kupeleka nchi jirani ambako kuna unafuu kidogo, angalau zile gharama alizotumia zirudi.

Alisema ujio wa mwekezaji huyo, utakuwa ni suluhisho pekee kwa wafugaji na mwanzo wa kuwa na vikundi vya wafugaji vitakavyowasaidia kuzalisha kwa tija na kukua kiuchumi mmoja mmoja.

Mfugaji mwingine, Amalia Mramba alisema kwa kuwa changamoto za wafugaji wa ng'ombe wa maziwa zinajulikana, elimu inahitajika ili waweze kuzalisha kwa tija kwa kuwa tayari



**"Changamoto tuliyonayo ni kutokuwa na vikundi vya wafugaji, hasa wa ng'ombe wa maziwa, kutokana na hali hii ilitulazimu kuchukua maziwa hapa na kwenda kuyauza Kenya."**
Edward Massawe, mfugaji

mwekezaji ameshapatikana.

"Soko sasa limepatikana, tunahitaji kupata elimu ya namna ya kuongeza uzalishaji kwa tija na kuhakikisha maziwa yanazalishwa kwa ubora wa hali ya juu ili tuweze kwenda mbali zaidi, mwanzo mzuri umeshaonekana baada ya kufungua kituo hiki cha maziwa hapa Rombo," alisema Mramba.

Akizungumzia uwepo wa kituo hicho cha kukusanyia maziwa, Meneja wa Kiwanda cha Maziwa cha Kondiki, Adrian Kimaro alisema kwa miaka 15 wamekuwa wakikusanya maziwa maeneo mbalimbali ya Mwika na Marangu.

Alisema baada ya kuona wafugaji wa vijiji hivyo wanatafuta soko la kuuzia maziwa wakaamua kuanzisha kituo hicho.

"Takribani miaka 15 tumekuwa tukikusanya maziwa maeneo ya Mwika na Marangu na sasa tumeongeza wigo hadi Rombo kwa lengo la kuongeza ukusanyaji wa maziwa na kuleta hamasa zaidi kwa wafugaji ili waweza kufuga ng'ombe wa maziwa wenye kuleta tija," alisema.

Pia, alisema kituo hicho kina uwezo wa kukusanya maziwa lita 500 kwa siku na wataendelea kuongeza wigo zaidi kwa sababu mahitaji ya maziwa yaliyosindikwa nchini yanaendelea kuongezeka.

Kimaro alisema hadi sasa wana wafugaji 1,000 waliopo Mwika na Marangu na kiwango cha maziwa wanachopata kutoka kwa wafugaji hao ni lita 6,500 hadi 8,000 kwa siku.

Robert Schozderk kutoka nchini Poland, ambaye ni mwezeshaji wa vikundi vya wakulima na wafugaji, alisema namna pekee ya wafugaji kuweza kufanikiwa ni kuwa na vyama vya ushirika wa maziwa na kwamba itasaidia wakulima kupata maendeleo zaidi.

"Ili kupata wafugaji wengi ni kuwa na vyama vya ushirika vyenye nguvu ili wafugaji waweze kuwa pamoja na kutengeneza kikundi chenye nguvu zaidi na kuungana kwa pamoja kwa kuwa na ubunifu mkubwa zaidi utakaoleta tija," alisema Schozderk.

Ofisa kilimo, mifugo na uvuvi wa wilaya hiyo, Emmanuel Martine alisema wilaya hiyo ina jumla ya mifugo 32,000 huku asilimia 75 hadi 89 ni ng'ombe wa maziwa.

# Wavuvi watishia kutolipa ushuru

**Na Said Hauni, Lindi**

UMOJA wa wavuvi na wachuuzi wa samaki mjini hapa, wamemtaka Mkurugenzi wa Halmashauri kutekeleza ahadi ya kukarabati paa la jengo wanalotumia kuuzia mazao yao vinginevyo wataitisha mgomo wa kutolipa ushuru.

Hayo yalielezwa mwishoni wa wiki na umoja huo baada ya barua iliyopelekwa kwa Mkurugenzi huyo, Juma Mnwele ikielezea dhamira hiyo kutokana na adha wanayopata ya kupigwa jua na kunyeshewa mvua kila siku.

Barua hiyo ya Desemba 18 mwaka huu iliyosainiwa na Mwenyekiti wa Umoja huo, Salehe Kazumari, inamtaka Mkurugenzi kutekeleza ahadi yake ya kurejesha paa hilo Desemba 10 mwaka huu.

Aidha, inaeleza kuwa kutokana na mateso wanayopata hawatakuwa tayari kulipa ushuru hadi uongozi ukarabati wa paa hilo, lililoezuliwa na upepo ulioambatana na mvua mwezi mmoja uliopita.

Barua hiyo inaeleza kuwa tangu upepo kuezua paa, wanapata mateso wakitekeleza majukumu yao

"Tulifika ofisini kwako kuleta taarifa na kutuahidi kuwa Desemba 10 kazi hiyo ingetekelezwa, lakini muda unazidi kupita na hakuna kinachoendelea zaidi ya kupeleka nguzo," alieleza Kazumari kwenye barua hiyo.

Aidha, barua imeeleza kuwa hadi Desemba 25 mwaka huu, bila kuona utekelezaji, Umoja ungetoa tamko la kutaka wavuvi na wachuuzi kutolipa ushuru wa Manispaa ambao ni asilimia tatu hadi ukarabati huo ufanyike.

Mkurugenzi wa Manispaa akijibu malalamiko ya Umoja huo, kupitia barua yake ya Desemba 19 mwaka huu, aliuomba uongozi kutozuia ushuru kwani urejeshaji wa paa ungefanyika ndani ya muda uliopangwa, hata hivyo hakuutaja muda huo.

Alisema pamoja na changamoto zilizopo Halmashauri ina jukumu la kutengeneza mazingira wezeshi ya kufanyia biashara kwa makundi ya wachuuzi wa samaki.

"Napenda kukufahamisha kuwa ukarabati wa eneo lililoezuliwa na upepo utafanyika ndani ya muda kama ilivyoahidiwa," ilieleza sehemu barua hiyo.

Novemba 15 mwaka huu, saa 8 mchana, mvua iliyoambatana na upepo iliezua paa la jengo linalotumiwa na wavuvi na wachuuzi wa samaki.

CamScanner